



TANGAZO

KUHUSU URASIMISHAJI WA MATUMIZI YA MBEGU ZA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI).

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) inapenda kuwataarifu wadau wote wanaojihusisha na uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa mbegu zinazomilikiwa na Taasisi kuwa ni wajibu wao kuhakikisha wanazingatia taratibu za haki miliki, ikiwemo kusaini mikataba rasmi ya matumizi (*Licensing Agreements*) na kulipa mirabaha stahiki kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 30 vikisomwa pamoja na Kifungu cha 40 cha Sheria ya Haki Miliki za Ugunduzi wa Mbegu za Mimea (*Plant Breeders' Rights Act*), pamoja na Kanuni ya 33(b) ya Kanuni za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, 2023, TSN. 448 la tarehe 30 Juni 2023.

Kwa mantiki hiyo, TARI inatoa wito kwa wazalishaji, wasambazaji, wauzaji, kampuni, taasisi na mtu yeyote anayejihusisha au anayetarajia kuanza kuzalisha, kusambaza au kuuza mbegu au teknolojia nyingine yoyote inayomilikiwa na TARI, kuwasiliana na Taasisi ndani ya kipindi cha siku thelathini (30) tangu tarehe ya kutolewa kwa tangazo hili kwa lengo la:

- i. Kujisajili
- ii. Kuhakiki na kuhuisha taarifa zao
- iii. Kusaini mikataba rasmi ya matumizi ya teknolojia na mbegu za TARI;
na
- iv. Kuweka utaratibu sahihi wa ulipaji wa mirabaha kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.

Baada ya kipindi hicho cha siku 30, TARI itachukua hatua za kisheria dhidi ya wadau wote watakaoshindwa kutekeleza wito huu.

Taarifa ziwasilishwe kwa anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI),
S.L.P. 1571,
Dodoma, Tanzania.
Barua pepe: dg@tari.go.tz**